Ubatizo, Ulitoka Kwa Mungu Au Wanadamu?

(Baptism, From God Or Man?)

Na

Ellis P. Forsman

Ubatizo, Ulitoka Kwa Mungu Au Wanadamu?

(Baptism, From God Or Man?)

Na

Ellis P. Forsman

Oktoba 10, 2011

Ubatizo, Ulitoka Kwa Mungu Au Wanadamu?

Mat. 21:23-27

Ni nani mwanzilishi wa maji yaa ubatizo? Ubatizo ulitoka kwa Mungu au wanadamu? Ubatizo ni muhimu kwa wokovu?

Haya ni maswali muhim inayohusisha wokovu kutoka dhambini. Biblia inatoa majibu!

Mamlaka Ya Ubatizo

Mamlaka ya maji ya ubatizo ni muhim. Mamlaka ya tendo lolote la kidini ni muhimu. Kuhoji mamlaka ya Kristo ni kuhoji mamlaka ya Mungu, mamlaka iliyojuu kuliko zote.

Yesu, Mwana wa Mungu alipata mamlaka yake toka kwa Mungu. Mara kabla hajarudi kwa Baba yake, Yesu aliwaambia wanafunzi wake katika Mat. 28:18, "*…Mamlaka yote nimepewa mbinguni na duniani.*"

Hivyo, Yesu, alifundisha kwa mamlaka ya Mungu. Alichokifundisha Yesu, Mungu alifundisha; alichofundisha Mungu, Yesu alifundisha.

Mamlaka ya Kristo mara nyingi inazidi ya mwanadamu. Kama mamlaka ya mwanadamu inazidi mamlaka ya Kristo, basi mwanadamu yuko juu ya Mungu. Hii itamfanya mwanadamu <u>hasitii</u> mamlaka yoyote.

Mtanziko Wa Wakuu Wa Makuhani & Wazee

Wakuu wa makuhani na wazee hekaluni wakati wa Kristo walijikuta katika mtanziko, wakinaswa na maswali yao wenyewe walipojaribu kuhoji mamlaka ya Kristo.

Mat. 21:23-27, "*Hata alipokwisha kuingia hekaluni, wakuu wa makuhani na wazee wa watu wakamwendea alipokuwa akifundisha wakasema, ni kwa amri gani unatenda mambo haya? naye ni nani aliyekupa amri hii? Yesu akajibu akawaambia, , na mimi nitawauliza neno moja ambalo mkinijibu nami nitawambia ni kwa amri gani ninatenda haya. ubatizo wa Yohana ulitoka wapi? Ulitoka mbinguni au kwa wanadamu? Wakahojiana wao kwa wao wakisema, tukisema ulitoka mbinguni, atatuambia mbona basi hamkumwamini? Na tukisema ulitoka kwa wanadamu, twaogopa mkutano maana watu wote wamwona Yohana*

kuwa ni nabii. Wakamjibu Yesu wakasema, hatujui. Naye akawaambia, wala mimi siwaambii ninyi ni kwa amri gani ninatenda haaya."

Kuna hitimisho tatu tunaweza kupata katika kifungu hiki.

- Kuna tofauti ya mamlaka kutoka kwa Mungu (mbingu) na mamlaka yatokayo kwa wanadamu.
- Mamlaka yatokayo kwa Mungu yanahitaji imani na utii.
- Mamlaka yatokayo kwa wanadamu ni ya kibinadamu, siyo ya kiungu, na ni badilifu.

Paulo mtume wa Kristo, anaweka wazi anatofautisha mamlaka ya Kristo na mamlaka ya wanadamu. Kuna tofauti kubwa kwamba mji wa milele mbinguni iko katika hatari.

Gal. 1:7-10, "*Wala si nyingine lakini wapo watu wawataabishao na kutaka kuigeuza injili ya Kristo. Lakini ijapokuwa sisi au malaika wa mbinguni atawahubiri ninyi injili yoyote isipokuwa hiyo tuliyowahubiri, na alaaniwe. Kama tulivyotangulia kusema na sasa, nasema tena, mtu yeyote akiwahubiri ninyi injili yoyote isipokuwa hiyo mliyoipokea, na alaaniwe. Maana sasa je ni wanadamu ninaowashawishi, au Mungu? Au nataka kuwapendeza wanadamu? Kama ningekuwa hata sasa nawapendeza wanadamu, singekuwa mtumwa wa Kristo.*"

Hakuna shaka juu ya hili. Mitume waliovuviwa walidaddavua swali juu ya mamlaka hayo ambayo tunapaswa kutii; hiyo ni, Mungu na sio mwanadamu!

Mungu Kupitia Yohana Mbatizaji

Mungu kwanza aliruhusu maji ya ubatizo kupitia Yohana Mbatizaji.

Yesu, Mwana wa Mungu, alitangaza katika Luka 16:16, "*Torati na manabii vilikuwapo mpaka Yohana; tangu wakati huo habari njema ya ufalme wa Mungu hutangazwa na kila mtu hujiingiza kwa nguvu.*"

"*Mpaka* Yohana," inaelezwa na Yesu ikionyesha kwamba uhusiano na Mungu kwa mwanadamu na wokovu wake ulibadilishwa kwa kuja kwake Yohana Mbatizaji.

Bwana wetu alisema, "*tokea wakati huo ufalme wa Mungu unahubiriwa,*" ambayo hakika, inasema kwamba injili ya ufalme ni kitu kimoja na sheria na manabii ni kitu kingine.

Yohana mwenyewe alisema katika Yoh. 1:17, "*Kwa kuwa torati ilitolewa kwa mkono wa Mungu; neema na kweli zilikuja kwa mkono wa Yesu Kristo.*"

"*Injili ya ufalme*" ilijumuishwa kwa mara ya kwanza, "*ubatizo kwa ajili ya ondoleo la dhambi.*"

Marko anaandika katika Marko 1:1-5, "*Mwanzo wa injili ya Yesu Kristo Mwana wa Mungu. Kama ilivyoandikwa katika nabii Isaya, tazama namtuma mjumbe wangu mbele ya uso wako, atakaye itengeneza njia yako. Sauti ya mtu aliaye nyikani, itengenezeni njia ya Bwana, yanyosheni mapito yake. Yohana alitokea akibatiza nyikani na kuhubiri ubatizo wa toba liletalo ondoleo la dhambi. Wakamwendea nchi yote ya Uyahudi, nao wa Yerusalemu wote, wakabatizwa katika mto wa Yordani, wakiziungama dhambi zao.*"

Yohana alihubiri ubatizo wa toba "*kwa ajili ya ondoleo la dhambi*" kama sehemu muhim ya injili ya ufalme.

Kwa vile ubatizo wa Yohana ulikuwa ni ubatizo wa toba "*kwa ajili ya ondoleo la dhambi,*"isingeweza kuwa kweli kwamba walibatizwa, wakikiri kwamba hawakuwa na dhambi.

Walibatizwa "*kwa ajili ya ondoleo la dhambi*," "*wakikiri dhambi zao*", ili waweze kupata msamaha wa dhambi zao.

Ubatizo ambao Yohana alifundisha ulitoka kwa Mungu, sio kwa wanadamu. Kama ubatizo wa Yohana ungetoka kwa wanadamu, ingeweza kuwa kama ubatizo nyingi ambaazo hufundishwa na wanadamu leo – unabatizwa kwa sababu tayari umeshaokolewa – au, batizwa ukikiri kwamba huna dhambi. Kunatofauti gani! Ubatizo umetoka kwa Mungu, au wanadamu?

Ubatizo Kutoka Kwa Mungu

Ubatizo kwa ajili ya ondole la dhambi haikuanzishwa na Yohana. Biblia inasema katika Luka 3:1-3, "*Mwaka wa kumi na tano wa kutawala kwa Kaisari Tiberio, Pontio Pilato alipokuwa liwali wa Uyahudi, na Herode mfalme wa Galilaya, na Filipo ndugu yake mfalme wa Iturea na nchi ya Trakoniti, na Lisania mfalme wa Abilene, wakati wa ukuhani mkuu Anasi na Kayafa, <u>neno la Mungu lilimfikia Yohana</u> mwana wa Zakaria, jangwani. Akafika nchi yote iliyokaribu na Yordani, <u>akihubiri ubatizo wa toba liletalo ondoleo la dhambi</u>,*"

Ubatizo wa maji kwa ajili ya ondoleo la dhambi ulianzishwa na Mungu, sio Yohana Mbatizaji. Yohana alihubiri kile alichoamriwa na Mungu ili ahubiri.

Hitimisho lazima ifikiwe katika kukumbuka wakuu wa makuhani na wazee, walipozingatia mtanziko wao.

Kukataa ubatizo kutoka kwa Mungu inaweza kuwa kutomwamini Mungu.

Kama kukataa ubatizo wa Yohana unamanisha kutoamini, hivyo kukataliwa kwa ubatizo ulioruhusiwa na Kristo kuokolewa kuna manisha kutoamini katika Kristo.

Yesu alisema katika Marko 16:16, "*Aaminiye na kubatizwa ataokoka asiyeamini atahukumiwa.*"

Je tuna mwamini? Kama mtu akikataa amri yake ya kubatizwa ili aokolewe, anajikuta katika nafasi iyo hiyo kama wakuu wa makuhani na wazee.

Kukataa ubatizo, inamanisha kutomwamini Mungu na Kristo walio ruhusu ubatizo. Kukataa ubatizo ni kumkataa Mungu na neno lake: Luka 7:30, "*Lakini Mafarisayo na wanasheria walilipinga shauri la Mungu juu yao, kwa kuwa hawakubatizwa naye.*"

Leo tunaweza kusikia wakisema, "Mhubiri Kristo na sio ubatizo." Lakini hiyo haiwezi kuwa kweli, hata ya Yohana Mbatizaji, aliyeandaa njia ya Kristo.

Yohana alitumwa kumbatiza Kristo, kama tunavyosoma katika sura ya 3 ya Mathayo. Kubatizwa kwa Yesu na Yohana ilikuwa ni kufanya mapenzi ya Mungu, kutimiza maagizo ya Mungu.

Yesu alitembea umbali wa maili 60 ili abatizwe na Yohana. Lakini Yohana anajibu katika Mat. 3:13-17, "*Wakati huo Yesu akaja kutoka Galilaya mpaka Yordani kwa Yohana ili abatizwe. Lakini Yohana alitaka kumzuia akisema, mimi nahitaji kubatizwa na wewe, nawe waja kwangu? Yesu akajibu akamwambia kubali hivi sasa; kwa kuwa ndivyo itupasavyo kuitimiza haki yote. Basi akamkubali. Naye Yesu alipokwisha kubatizwa mara akapanda kutoka majini; na tazama mbingu zikamfunukia, akamwona Roho wa Mungu akishuka kama hua, akija juu yake; na tazama sauti kutoka mbinguni ikisema, huyu ni Mwanangu , mpendwa wangu, ninayependezwa naye.*"

Yesu alimpa Yohana habari kwamba hili lilikuwa jambo la pekee – "teseka sasa"; kwamba ilikuwa muhim "*kutimiza haki yote*" – kutii maagizo yote ya Mungu.

Daudi alisema katika Zab. 119:172, "*Ulimi wangu na uimbe ahadi yako, maana maagizo yako yote ni ya haki.*"

Hivyo, ubatizo wa Yesu ulitoka kwa Mungu, na Yesu alitimiza maagizo yote ya Mungu yeye mwenyewe akitimiza haki yote. Aliwajibika kumtii Baba yake kwa kubatizwa.

Ilikuwa baada ya kubatizwa kwamba sauti ikaja kutoka mbinguni ikisema katika Mat. 3:17, "*…Huyu ni Mwanangu, mpendwa nipendezwaye naye.*"

Yesu, Ubatizo, Wokovu

Yesu Kristo, Mwana wa Mungu, aliagiza ubatizo kama msingi wa wokovu, akitangaza kwamba mamlaka yote, mbinguni na duniani, amepewa yeye.

Yesu aliamuru katika Mat. 28:18-20, "*Yesu akaja kwao akasema nao, akawaambia nimepewa mamlaka yote mbinguni na duniani. Basi enendeni mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi, mkiwabatiza kwa jina la Baba, na Mwana, na Roho Mtakatifu; na kuwafundisha kuyashika yote niliyowaamuru ninyi. Na tazama mimi nipo pamoja nanyi siku zote, hata ukamilifu wa dahari.*"

Marko akaandika maneno haya katika Marko 16:15-16, "*Akawaambia enendeni ulimwenguni mwote mkahubiri Injili kwa kila kiumbe. Aaminiye na kubatizwa ataokoka, asiyeamini atahukumiwa.*"

Agizo la kubatizwa lilitoka kwa Mungu, kupitia Yohana Mbatizaji, kupitia Yesu Kristo, na kupitia mitume wake. Mlolongo unafuata hivi:

- Yohana alifanya wanafunzi, akiwabatiza "*kwa ajili ya ondoleo la dhambi.*" (Marko. 1:1-5).
- Yesu mwenyewe alifanya wanafunzi kwa kuwafanya wabatizwe.
    * Yoh. 3:26, "*Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu hata akamtoa Mwanawe pekee ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele.*"
    * Yoh. 4:1-2, "*Kwa hiyo Bwana alipofahamu ya kuwa Mafarisayo wamesikia ya kwamba, Yesu anafanya wanafunzi wengi kuliko Yohana, na kuwabatiza, (lakini Yesu mwenyewe hakubatiza, bali wanafunzi wake,)*"
    * Mat. 28:19, "*Basi enendeni mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi, kiwabatiza kwa jina la Baba, na Mwana, na Roho Mtakatifu;*"
    * Marko 16:16, "*Aaminiye na kubatizwa ataokoka, asiyeamini atahukumiwa.*"
- Mtu hawezi kuwa mwanafunzi wa Yesu kama hajabatizwa.
- Mtu hawezi kuondolewa dhambi kama hajabatizwa.

Ubatizo Unatoka Kwa Mungu, Siyo Kwa Mwanadamu, Kwa Ajili Ya Ondoleo La Dhambi

Mdo. 2:38, "*Petro akawaambia tubuni mkabatizwe kila mmoja kwa jina lake Yesu Kristo, mpate ondoleo la dhambi zenu nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu.*"

Wengi katika ulimwengu wa dini wanadai kwamba maana ni "ubatizwe kwa sababu dhambi zako zimeondolewa." Wanakiuka neno la Mungu kwa sababu ya kitu wasichopenda kufanya. Hawaamini neno la Mungu, kama ilivyokuwa kwa wakuu wa makuhani na wazee kuhusu ubatizo wa Yohana Mbatizaji.

Wanafanya madai kwamba neno "kwa ajili" inamanisha "kwa sababu". Hebu tuangalie wazo hilo kwa karibu.

Mat. 26:26-28 inasema, "*Nao walipokuwa wakila Yesu alitwaa mkate, akabariki akaumega, akawapa wanafunzi wake akasema, twaeni mle huu ndio mwili wangu. Akakitwaa kikombe akashukuru akawapa akisema, nyweni nyote katika hiki; kwa maana hii ndiyo damu yangu ya agano imwagikayo kwa ajili ya wengi kwa ondoleo la dhambi.*"

Kama neno "*kwa ajili ya ondoleo la dhambi*" hakika inamanisha "kwa sababu dhambi zako zimeondolewa", basi msitari huu ungesomeka hivi: "Maana hii ndio damu yangu ya agano jipya, imwagikayo kwa sababu dhambi zao zimeondolewa tayari."

Kama dhambi zao zilikuwa tayari zimeondolewa, kwa nini Yesu alimwaga damu yake?

Kama neno "kwa ajili" katika Mdo. 2:38 ina manisha "kwa sababu" (mlibatizwa kwa sababu tayari dhambi zenu zimeshaondolewa) basi Yesu alimwaga damu yake "kwa sababu" dhambi zao tayari zilikuwa zimeshaondolewa. Ndugu na dada, hii kutafsiri kimakosa na maana ya maandiko. Yesu alimwaga damu yake ili kuondoa dhambi zetu. Neno katika kifungu hiki inatafsiriwa hivi "kwa ajili" ya ondoleo la dhambi.

3000 waumini waliotubu waliopata msamaha wa dhambi zao, kama ilivyoandikwa katika sura ya pili ya Matendo ya Mitume, hawakupokea msamaha wa dhambi hapo nyuma kabla ya injili ya Petro. Mdo. 2:37, "*Walipoyasikia hayaa wakachomwa mioyo yao, wakamwambia Petro na mitume wengine, tutendeje ndugu zetu?*

Mara nyingi, jambo liliwa ni "*kwa ajili ya ondoleo la dhambi".* Hawakupokea msamaha wa dhambi zao kwa kumwamini Bwana tu na kumkubali Kristo kama Mwokozi wao binafsi.

Walipokea msamaha wa dhambi zao walipotii agizo lililovuviwa na Mungu kupitia Petro katika Mdo. 2:36-41, "*Basi nyumba yote ya Israeli*

na wajue yakini ya kwamba Mungu amemfanya Yesu huyo mliyemsulubisha kuwa Bwana na Kristo. Walipoyasikia haya wakachomwa mioyo yao wakamwambia Petro na mitume wengine, tutendeje ndugu zetu? Petro akawaambia, tubuni mkabatizwe kila mmoja kwa jina lake Yesu Kristo, mpate ondoleo la dhambi zenu nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu. Kwa kuwa ahadi hii ni kwa ajili yenu, na kwa watoto wenu, na kwa watu wote walio mbali, na kwa wote watakaoitwa na Bwana Mungu wetu wamjie. Akawashuhudia kwa maneno mengine mengi sana na kuwaonya akisema jiokoeni na kizazi hiki chenye ukaidi. Nao waliolipokea neno lake wakabatizwa; na siku ile wakaongezeka watu wapata elfu tatu."

Hitimisho

Mungu au mwanadamu?

Mwanadamu anawajibika kwa Mungu. Mitume wa Kristo, ambao ndio wenye mamlaka wa Mungu duniani, alisema katika Mdo. 5:29, "*Petro na mitume wengine wakajibu wakisema, imetupasa kumtii Mungu kuliko wanadamu.*"